

**SHULE YA UPILI YA GATITU S.L.P. 01030, 327, GATUNDU**  
**MTIHANI WA MWISHO WA MWAKA (2014) KIDATO CHA TATU**  
**KARATASI YA FASIHI 102/3**

JINA.....DARASA.....NUMB.....

**A.Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

**USAWA**

Waume msiudhike, swali nawauliza,  
Wala msibabaike, hadhi yetu twatetea,  
Kuwatweza wanawake, hamuoni mwakosea?  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Si vizuri kuwatesa, wana wake kuonea,  
Kuwapiga pasi kosa, kwa hakika ni hatia,  
Nyote mna sawa hisa, katika hii dunia,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Mngakaa mfikiri, lau kwa miaka mia,  
Na muwache ujabari, wanawake si ngamia,  
Sidanganywe na mahari, msambe ni kununua,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Madharau huwa mengi, kwa waume narudia,  
Huwawekea vigingi, wanawake kila njia,  
Kwa waume hawasongi, fikira zao kutoa,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Usawa tunautaka, si hivi kubagua,  
Tufanye mambo shirika, hakuna wa kubakia,  
Kubaki nyuma twachoka, waume kutangulia,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Kila alo mwanadamu, kwa muumba katokea,  
Kwani wote wanadamu, ni wamoja wa hisia,  
Bora wote kuheshimu, bila umbo kutengwa,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Usawa tunautaka, si wa umbo na kuvaa,  
Wala si wa kugeuka, kuota ndevu vifua,  
Ni ule wa kutukuka, kwenye utu na tabia,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Wengine wana shutuma, mabibi kushambulia,  
Roho zao ni tamima, ni wepesi wa kulia,  
Hawawezi kusimama, vita vinapotokea,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Waume vuta akili, nguvu si kujivunia,  
Mnapaswa kubadili, dhana zenu na tabia,  
Hakuna mtu dhalili, elimu yetu sawia,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

Nimeutaja usawa, nadhani mmesikia,  
Kama sahani na kawa, pima utu na hisia,  
Kwa ujenzi twatakiwa, kina mama na raia,  
Wanawake wawe sawa, na waume duniani.

**Maswali**

(a) Eleza falsafa ya mshairi. (alama 3)

.....  
.....  
.....

(b) Kulingana na shairi hili kwa nini mshairi anadai usawa? (alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

(c) Kwa kutolea mifano miwili, fafanua idhini ya mshairi. (alama 2)

.....  
.....

(d) Eleza sura ya shairi hili.

(alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

(e) Mwandishi ametumia mbinu gani za lugha kuwasilisha ujumbe wake?

(alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

(f) Eleza maana ya maneno yafuaatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili.

(Alama 3)

(i) Kuwatweza:.....

(ii) Kuwapinga pasi kosa:.....

(iii) Vigingi:.....

**B. Eleza maana ya istilahi hizi za fasihi simulizi.**

(alama 8)

i)Miviga:.....  
.....

ii)Mighani:.....  
.....

iii)Visasili:.....  
.....

iv) Wawe

.....  
.....

(b) Fafanua sifa nne za miviga.

(Alama 4)

.....  
.....  
.....

(c) i. Fafanua dhima ya kifunguzi katika utambaji wa hadithi.

(Alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

ii) Eleza sifa Nne za fanani katika utambaji.

(Alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

C. "Sitaki kelele hapa kwa Ikulu ya raisi.

"Alaa! Bwana mdogo hata wewe ushaletwa humu Ikuluni?"

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.

(Alama 4)

.....  
.....  
.....  
.....

b) Eleza mbinu mbili za kimtindo zilizojitokeza katika dondoo hili.

(Alama 2)

.....  
.....  
.....



